

Timu ya waratibu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, wilaya ya Ileje imetembelea na kukagua vituo ambavyo vitatumika katika zoezi za kuandikisha wapiga kura , katika kata mbalimbali wilayani hapa kwa ajili ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajia kufanyika hapo Novemba 27,2024.

Sambamba na kukagua vituo hivyo, timu hiyo imeshiriki katika kutoa hamasa kwa wananchi kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika daftari la wapiga kura ili waweze kushiriki katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa ili kupata viongozi walio bora.

Aidha timu hiyo imetoa rai , watendaji wa Kata pamoja na Vijiji kuendelea kutoa hamasa kwa wananchi katika ngazi ya kata na vijiji ili wajiandikishe na kushiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa.Zoezi la kuandikisha wapiga kura litaanza rasmi tarehe 11 oktoba hadi tarehe 20 ya mwezi oktoba 2024.